

UVUNAJI WA VIAZI VITAMU

Viazi vitamu hukomaa kwa mda wa miezi mitatu hadi minne kutegemeana na aina ya mbegu.

ZIFUATAZO NI DALILI ZA VIAZI VITAMU KUKOMAA

- Majani kuwa njano
- Kukauka kwa mmea
- Kutoka utomvu kwenye viazi
- Mipasuko kwenye tuta

MAVUNO

Hutegemea aina ya mbegu (15 ta/ha)



CIP
INTERNATIONAL
POTATO CENTER



CGIAR

Tanzania Agricultural Research Institute (TARI) - Ukiriguru



S.L.P 1433, Mwanza,



cdukiringuru@tari.go.tz



www.tari.go.tz



+255 735 983 106



+255 735 983 104

KILIMO BORA CHA CHA VIAZI VITAMU



Umuhimu wa Viazi vitamu

Ni zao la chakula na biashara, Ni chanzo cha Vitamini A, wanga na nyuzinyuzi. Vitamini A husaidia uono mzuri na ukuaji wa watoto, wazee na wajawazito. Wanga husaidia kuupa mwili nguvu. Nyuzinyuzi husaidia kurahisisha mmeng'eno wa chakula hivyo huepusha uwezekano wa kansa ya utumbo mpana

Aina za mbegu za viazi vitamu



- ◆ Viazi karoti (Viazi lishe); Vina kiwango kikubwa cha vitamini A
- ◆ Viazi vya kawaida; Hivi ni vyeupe au kri-mu kwa ndani, vina kiwango kikubwa cha wanga
- ◆ Viazi zambarau huboresha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa

Mahitaji ya uzalishaji wa Viazi

- ◆ Mvua za wastani (750 mm) kwa mwaka
- ◆ Joto la wastani
- ◆ Udongo tifuftu usio na chumvichumvi

Mambo ya kuzingatia

Maandalizi ya shamba

Shamba linatakiwa litifuliwe vizuri ili kuwezesha mizizi kupenya vizuri

Ubora wa mbegu

Mbegu zinatakiwa kuwa na macho kuanzia 5 - 8 na isiwe na mashambulizi ya magonjwa

Nafasi ya upandaji

Kati ya mmea na mmea ni 30 cm na kati ya tuta na tuta au mstari ni mita moja (1m)

Unyevu wakati wa upandaji

Shamba linatakiwa kuwa na unyevu kiasi ili kuwezesha mimea kuota vizuri

Matumizi ya mbolea

Mbolea ya asili (Samadi) tani 5 hadi 10 kwa



Kuhudumia shamba

Dhibiti magugu, palizi moja au mbili zinatoshwa kutegemeana na aina ya udongo na hali ya hewa.



Dhibiti mashambulizi ya wadudu kwa kufukia mipasuko shambani

Kagua shamba lako mara kwa mara kuangalia mashambulizi ya magonjwa. Kama kuna mimea imeathirika na magonjwa ya virusi ngichoma moto au fukia.